JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

# SHERIA BULLETIN

Toleo la 14

*Mafanikio ya*

# MIAKA 3

ya Rais **SAMIA** kupitia **MoCLA**



## YALIYOMO



Muhtasari wa mafanikio ya Wizara.. Uk. 02


MSLAC: Mikoa Saba ya utekelezaji.. Uk. 05


Tanzania yasifika kwa kupokea wakimbizi.. Uk. 07


OWMS yaokoa trilioni 3.4 kupitia mashauri.. Uk. 08



## BODI YA UHARIRI

**DKT. KHATIB KAZUNGU**
Naibu Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
William Mabusi | Hyasinta Kissima | Josephat Kimaro

**WASANIFU WA KURASA:** Waziri Bosco, Lusajo Mwakabuku



# Muhtasari wa Mafanikio ya MoCLA kwa miaka 3

**Na Lusajo Mwakabuku**
- WyKS Dodoma

### Msaada wa Kisheria

Serikali inatekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign - MSLAC). Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

Kampeni imekwishatekelezwa katika mikoa saba ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida na Njombe Katika Mikoa hii, jumla ya Halmashauri 48, Kata 520, Vijiji na Mitaa 1,539 ilifikiwa wakati wa utekelezaji.

Aidha, jumla ya wananchi 493,638 (Wanaume 251,453 wanawake 242,185) walifikiwa katika ngazi za vijiji na kata na wafungwa na mahabusu 7570 (Wanaume 7,211 wanawake 359) walifikiwa katika maeneo ya vizuizi. Kampeni hii ni endelevu na inatarajiwa kuwafikia wananchi katika mikoa yote, Tanzania Bara na Zanzibar.

### Vikao vya Kikanda na Kimataifa Katika Sekta ya Sheria

Tanzania ilikuwa nchi mwenyeji wa Kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Katika kikao hicho jumla ya wadau 1,507 wameshiriki. Yapo manufaa ambayo Tanzania imenufaika kwa kuwa nchi mwenyeji wa Kikao hiki ikiwemo kuingiza fedha za kigeni takribani Dola za Marekani 7,000,000.



Rais Mwinyi akizindua kikao cha 77 cha Haki za Binadamu na Watu Arusha

Mwanzoni mwa mwaka huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Jumuiya ya Madola. Mkutano huo ulifanyika kuanzia tarehe 04 hadi 08 Machi, 2024 Unguja, Zanzibar. Jumla ya wageni 188 kutoka katika nchi 34 Wanachama wa Jumuiya ya Madola walishiriki. Yapo manufaa ambayo Tanzania imenufaika kwa kuwa nchi mwenyeji wa Kikao hiki ikiwemo kuingiza fedha za kigeni takribani Dola za Marekani 540,000.

Manufaa mengine ya Tanzania kuwa nchi mwenyeji wa mikutano ya kikanda na kimataifa katika Sekta ya Sheria ni pamoja na: -

(i) Kuongezeka sifa na heshima kwa Tanzania kidiplomasia na kuimarisha uhusiano wa kimataifa;

(ii) Tanzania kuendelea kuaminika na kuheshimika kimataifa katika kutambua na kuheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu; na

(iii) Kufahamika kwa vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania na hivyo kuongezeka kwa idadi ya watalii siku zijazo.

### Kuimarisha Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Kutoa Huduma za Kimahakama na Kwenye Uandishi wa Nyaraka za Kisheria.

Serikali inaendelea na uhakiki wa




Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akizindua kampeni ya MSLAC Dodoma

sheria zilizokamilika kutafsiriwa kwa mara ya kwanza ambapo jumla ya Sheria 258 zimekamilika tafsiri ya awali. Sheria hizo zitatangazwa rasmi ili zianze kutumika ili kuwawezesha Watanzania kuelewa sheria zilizopo na hivyo kuwarahisishia kupata haki na kutekeleza wajibu wao.

## Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki

(a) Kituo cha Huduma kwa Wateja

Ili kuimarisha upatikanaji Haki, Serikali imeanzisha Kituo cha Huduma (Contact Centre) kwa wateja kwa ajili ya kupokea malalamiko, uhitaji wa huduma za kisheria, taarifa na maoni kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali masuala ya haki. Kupitia Kituo hiki wananchi wenye changamoto za masuala ya kisheria wanaweza kuwasiliana na wataalam na hivyo kupatiwa msaada kupitia namba 0262160360.

(b) Ongezeko la Majaji

Ili kuongeza kasi ya kusikilizwa na kuhitimishwa kwa mashauri katika ngazi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, katika kipindi cha Machi, 2021 hadi Februari, 2024 jumla ya majaji 61 wameteuliwa. Kati yao, majaji 19 ni wa Mahakama ya Rufani na Majaji 42 ni wa Mahakama Kuu. Hivyo, hadi Februari, 2024 kuna jumla ya Majaji 135 (Mahakama Kuu 100 na Mahakama ya Rufani 35) ikilinganishwa na Majaji 74 (Mahakama Kuu 58 na Mahakama ya Rufani 16) waliokuwepo Machi, 2021.

(c) Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama

Kati ya Machi, 2021 na Februari, 2024 jumla ya Mahakama za Mwanzo 22 zimejengwa katika maeneo yafuatayo: Mtae (Tanga), Mkunya (Newala), Msanzi (Rukwa), Uyole (Mbeya), Mlimba (Morogoro), Mang'ula (Morogoro), Mtowisa (Rukwa), Laela (Rukwa), Haydom (Manyara), Ngerengere (Morogoro), Kimbe (Tanga), Nyakibimbili (Kagera), Matiri (Ruvuma), Kabanga – (Kagera), Chanika (Dar es Salaam), Mahenge (Kilolo Iringa), Mahenge (Morogoro), Luilo (Ludewa Njombe), Kinesi (Rorya Mara), Newala (Mtwara), Usevya (Katavi) na Madale (Dar es Salaam).



*Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kupokea malalamiko, uhitaji wa Huduma za Kisheria, taarifa na maoni (Contact Center)*

(d) Maboresho ya Mifumo ya TEHAMA ya Huduma za Mahakama

• Mfumo wa e-CMS

Mfumo wa Kielektroniki wa Kusimamia na Kuratibu Mashauri (e-Case Management System) umeanza kutumika kuanzia Novemba, 2023. Mfumo huo umeongeza ufanisi wa utendaji wa Mahakama na unafaida zifuatazo:-

(i)Umerahisisha usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao kupitia fomu maalumu ambazo zinapatikana moja kwa moja kwenye mfumo.

(ii) Umerahisisha upangaji wa mashauri, kwa kuwa unapanga mashauri moja kwa moja (automatic case assignment).

(iii)Kupatikana kwa wakati mienendo ya mashauri na nakala za hukumu.

(iv)Kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na Taasisi za Utoaji Haki.

(v)Unapunguza gharama za usikilizaji wa mashauri kwa Mahakama na wadau.

• Mfumo wa TTS

Mfumo huo una uwezo wa kutafsiri kumbukumbu za kimahakama kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na Kiswahili kwenda Kiingereza. Hadi sasa, mfumo umefungwa katika Mahakama 11 nchini ambapo katika kila Mahakama zimefungwa seti 4 za vifaa vya kuwezesha kutumika kwake.

## Kuimarisha Njia Mbadala za utatuzi wa Migogoro

Hadi Februari, 2024 wapo Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala 576. Kati ya hao, Waendesha Maridhiano ni 38, Watoa Huduma za Majadiliano ni 60, Wapatanishi ni 185 na Wasuluhishi ni 293 ikilinganishwa na Watatuzi wa Migogoro kwa Njia Mbadala 153 waliokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2021 wakiwemo Waendesha Maridhiano 5, Watoa Huduma za Majadiliano 15, Wapatanishi 50 na Wasuluhishi 83 waliokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2021.

## Uzingatiwaji wa Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kutokana na Tanzania kuzingatia masuala ya haki za binadamu na utawala bora ikiwa ni pamoja na Serikali kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Machi 2023, Taasisi Inayosimamia Haki za Binadamu Duniani (Global Alliance of National Human Rights Institutions – GANHRI Sub Committee on Accreditation) imeipatia Daraja "A" Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.



# UTEKELEZAJI WA **MSLAC** KWA MIKOA SABA

**Mama Samia Legal Aid Campaign**

## LENGO KUU

Kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini.

MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

## MALENGO MAHSUSI

- Kuongeza uelewa wa kisheria na haki za binadamu kwa jamii hususan haki za wanawake na watoto;
- Kuimarisha huduma ya ushauri wa kisheria na unasihi kwa waathirika na manusura wa ukatili wa kijinsia;
- Kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za kisheria;
- Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya sheria kwa umma, masuala ya haki na wajibu na misingi ya utawala bora;
- Kuwa na huduma endelevu za msaada wa kisheria katika ngazi zote za kijamii;

## WALIOHUDUMIWA

| Maeneo yaliyofikiwa | Wanufaika kwa ujumla | Mahabusi & Wafungwa | Magereza & Polisi | Huduma za RITA |
|---|---|---|---|---|
| Halmashauri: **48** | Wanaume: **251,453** | Wanaume: **7,211** | Magereza: **24** | Wanaume: **2,637** |
| Kata: **520** | Wanawake: **242,185** | Wanawake: **359** | Vituo vya Polisi: **28** | Wanawake: **2,608** |
| Vijiji/Mita: **1,539** | Jumla: **493,638** | Jumla: **7,570** | Jumla: **52** | Jumla: **5,245** |


## HUDUMA ZILIZOTOLEWA


Elimu kwa Umma juu ya masuala ya mirathi na wosia, ndoa, ukatili wa kijinsia, ulinzi wa watoto, umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi, masuala ya usafirishaji haramu wa binadamu;
Ushauri wa kisheria; Unasihi;
Kuandaa nyaraka za kisheria/kimahakama kwa wahitaji;
Kuwaunganisha wahitaji wa huduma na watoa huduma;
Usuluhishi wa mashauri/ migogoro; na
Kugawa vipeperushi vya elimu ya sheria kwa wananchi.









# UTATUZI WA MIGOGORO






*Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akihutubia kwenye Uzinduzi wa Mama Samia Legal Aid Campaign, tarehe 22 Julai, 2023, Viwanja vya Majimaji Songea.*

# Serikali kuendelea kutatua kero za wananchi.

**Na William Mabusi**
- WyKS Dodoma

*"Kliniki hii na zingine zitakazoendelea kuratibiwa na Serikali zimelenga kutoa suluhisho ya kero zenu, kumwezesha mwananchi kupata huduma bora kwa wakati na kuongeza utengamano na utulivu na hivyo kuchochea maendeleo ya jamii."*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi amewahakikishia wananchi kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha inatatua kero na changamoto zao katika kuimarisha utengamano na utulivu nchini. Dkt. Feleshi aliyasema hayo alipokuwa anazindua Kliniki ya kutoa ushauri na elimu ya sheria iliyoandaliwa na Ofisi yake, tarehe Juni 26, 2024 katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Jijini Dodoma. Kliniki hiyo ilifanyika kwa wiki nzima kuanzia Juni 26 hadi Julai 03, 2024.

"Kliniki hii na nyingine zitakazoendelea kuratibiwa na Serikali zimelenga kutoa suluhisho ya kero zenu, kumwezesha mwananchi kupata huduma bora kwa wakati na kuongeza utengamano na utulivu na hivyo kuchochea maendeleo ya jamii. Mahala pasipokuwa na masikilizano na kuwepo namna ya kujadili changamoto au kero mara nyingi kunakuwa na fukuto ambalo hupelekea maendeleo yasifikiwe kwa wakati lakini pia husababisha uadui kwani miongoni mwa pande zilizo katika mgogoro hupoteza mali, haki na hata maisha." Alisema.



Alitoa rai kwa Mawakili wa Serikali na Wadau wote wa sheria kujitofautisha na majukwaa mengine ya watetezi wa haki za binadamu kwa kutatua kero za wananchi na siyo kupapasa kero zao. Akitaja lengo la Wadau wote wa sheria ni kushughulikia kero za wananchi na si kuwaacha waangukie mikononi mwa watu wengine wasio na utaalamu wa sheria na mwisho kushindwa kutatuliwa kero zao kwa ukamilifu.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema uanzishwaji wa Kliniki za sheria ni takwa la Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia ni utekeleza ji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais ambao wamekuwa wakiyatoa kwenye hotuba zao wakikumbusha viongozi kushughulikia kero za wananchi kwa wakati ili kuepusha

**"Uanzishwaji wa Kliniki za sheria ni kutekeleza maelekezo ya Katiba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwatumikia wananchi lakini pia ni utiifu wa kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais wa Dkt. Philip Mpango"**

*Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi*
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

migogoro hiyo kwenda mahakamani ambako kuna gharama ya muda, gharama za ushindani kwa sababu mahakamani ni pande mbili zinapigania haki na moja lazima ishinde.

Akitoa salaam katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo alisema kupitia Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wananchi wameendelea kuangaliwa kwa jicho la pekee katika mageuzi yanayofanywa na Serikali ya kuboresha huduma za sheria kwa kuzisogeza karibu zaidi na waliko wananchi ili kero zao ziweze kutatuliwa kwa wakati.
Aidha, Bi. Makondo ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuiwezesha Wizara na Taasisi zake katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kuwatumikia wananchi. Akitumia mfano wa Kampeni ya Msaada wa Sheria ya Mama Samia na kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwemo mfumo wa Usajili Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria na kuanzisha Kituo cha kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kwa njia ya simu - Call centre. Namba maalum inayotumika katika Kituo hicho ni 026 2160360.
Makamu wa Rais wa Dkt. Philip Mpango, akizindua utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign mkoani Ruvuma tarehe 22 Julai, 2023 mjini Songea aliagiza kufanyika kwa uchambuzi wa kina wa masuala yanayoibuliwa kwenye utekelezaji wa kampeni hiyo tangu ilipoanza kutekelezwa na kuwekewa mkakati wa kuyapatia ufumbuzi.
Aliyataja baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa na changamoto na kuleta migogoro mingi kwa wananchi kuwa ni pamoja na migogoro ya umiliki wa ardhi, migogoro ya wakulima na wafugaji, kesi za madai ya mirathi, ukatili wa kijinsia na migogoro ya kazi na ajira.



Meza Kuu kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya uzinduzi wa Kliniki ya sheria, Juni 26, 2024 Viwanja vya Mwalimu Nyerere,



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akimsikiliza Mwenyekiti wa Umoja wa Wataafu Tanzania wanaolipwa na Hazina mzee John Joseph Kanyeto akitoa kero yake kabla ya kuzindua Kliniki ya sheria, Juni 26, 2024 Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dodoma.



# Zaidi ya watoto **Milioni 10** wasajiliwa RITA





**Na Josephat Kimaro**
**-** RITA

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) imekamilisha kusimika Mpango wa Usajili kwa Watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano katika Mikoa yote Tanzania Bara ambapo mpaka sasa zaidi ya watoto 10,236,651 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa kote nchini.

Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bw. Frank Kanyusi ameeleza kwamba mpango huu umeweza kusajili idadi hiyo ya watoto kwa sababu huduma hii imesogezwa na inapatikana karibu na makazi ya wananchi BILA MALIPO ambapo wananchi wanapata huduma hii katika maeneo mawili ambayo ni katika Vituo vya Tiba vinavyotoa huduma ya Mama na Mtoto na Katika Ofisi za Watendaji Kata kote nchini. Bw. Kanyusi amefafanua kwamba utekelezaji wa Mpango huu katika mkoa wa Dar es Salaam umeanza mwezi Disemba 2023 na sasa Wakala unaendelea kusimamia na kuhakikisha unafanyakazi kikamilifu katika mkoa huo na mikoa mingine yote ili kila mtoto anayestahili apate huduma.

Amefafanua kwamba utekelezaji katika kila Mkoa umefanyika katika hatua mbili ambapo hatua ya kwanza ni kufanya kampeni ya kuondoa bakaa la watoto wenye umri chini ya miaka mitano wasio na vyeti vya kuzaliwa na baada ya hapo hatua ya pili ni kuendelea kuwasajili watoto mara tu wanapozaliwa alimradi wasizidi siku tisini (90). Msisitizo huu unalenga kuzuia bakaa la baadaye; yaani wasiwepo watoto ambao hawakusajiliwa wakati tunatekeleza mpango huu maalum na ambao ni wa kudumu.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wakala umefanikiwa kusimika Mpango huu katika mikoa Sita ambayo ni Katavi, Rukwa, Tabora, Kagera, Kigoma pamoja na Dar es Salaam.

“Ni vizuri ieleweke kwamba usajili ni haki ya msingi ya kila mtoto na pia ni utambulisho wa kwanza wa msingi ambao unamuwezesha mtoto kupata cheti cha kuzaliwa. Cheti cha kuzaliwa ni nyaraka inayomuwezesha mtoto kupata huduma nyingine nyingi za msingi ambazo ni pamoja na kupata elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu; huduma za bima ya afya; kupata




*Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bw. Frank Kanyusi akimkabidhi cheti cha kuzaliwa mmoja wa wateja waliofika katika banda la RITA kupata huduma ya cheti cha kuzaliwa jijini Dar es salaam.*

ajira katika taasisi za umma na binafsi na manufaa mengine mengi," ameeleza Bw Kanyusi. Amefafanua zaidi umuhimu wa usajili wa vizazi na kusema kwamba taarifa zinazokusanywa na RITA katika utaratibu wa kusajili vizazi ni takwimu muhimu zinazoiwezesha Serikali kupanga mipango sahihi ya maendeleo, usambazaji wa huduma za kijamii na hata kupanga makazi bora kwa wananchi wake.

Kuanzishwa kwa mpango huu ni sehemu ya Mkakati wa Serikali pamoja na Wadau wa Maendeleo katika kuimarisha mifumo ya utambuzi wa wananchi wake. Kwa hiyo usajili wa vizazi ni mfumo wa kwanza unaomtambua mwananchi mara tu anapoingia duniani na taarifa zake kuweza kutumika katika mifumo mingine ya utambuzi kila inapohitajika kuthibitisha mahali mwananchi huyo alipozaliwa, umri wake, ni nani wazazi wake na nyinginezo, amefafanua Bw. Kanyusi.

Kabla ya kuanza Mpango huu, watoto walikuwa wanaweza kupata huduma hii ya usajili kwa kufika katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya tu, jambo ambalo lilikuwa ni changamoto kwa wananchi wengi kwani baadhi ya maeneo wanayoishi wananchi hao yako mbali sana na Ofisi za Wakuu wa wilaya, na hivyo kuongeza gharama za kupata huduma hii. Hali hiyo ilisababisha wazazi wengi kushindwa kuwasajili watoto wao.




*Wateja mbalimbali waliojitokeza katika mabanda ya kutolea huduma ya RITA katika Kampeni ya Msaada wa KIsheria ya Mama Samia - (MSLAC)*

Bw Kanyusi ameeleza kuwa kwa sasa kuna vituo vya usajili wa watoto vipatavyo 11,193 kote nchini, na kuongeza kuwa sasa RITA inaamini kuwa kila mzazi anaweza kumsajili mtoto na kupata cheti cha kuzaliwa pasipo usumbufu wowote. "Tunaamini kwamba kupitia Mpango huu Wakala utaweza kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuhakikisha kila mtoto amesajiliwa kufikia mwisho wa mwaka 2025,"ameeleza na kuongeza:. "Serikali tunajivunia mapinduzi haya makubwa yanayowahakikishia watoto kupata haki yao ya msingi ya kutambuliwa. Aidha Serikali kwa sasa imejikita katika kuimarisha mfumo huu na kuhakikisha watoto wanasajiliwa kwa wakati na ninaamini kadri siku zinavyoenda idadi ya watu waliosajiliwa itaendelea kuongezeka nchini." Akizungumzia jinsi huduma inavyotolewa katika vituo vya usajili, Bw. Kanyusi ameeleza kwamba mzazi anatakiwa kufika katika kituo cha usajili akiwa na nyaraka zinazomtambulisha mtoto hasa kadi ya kliniki na atahojiwa na Msajili kwa ajili ya kutoa taarifa muhimu za mtoto na wazazi wake. Taarifa hizo zitajazwa katika fomu maalumu na baada ya hapo mzazi au mlezi atapatiwa cheti. Baada ya hatua hiyo kukamilika, Msajili anaingiza taarifa za mtoto katika simu janja iliyowekwa mfumo maalumu na kuzituma kwenda katika kanzidata ya RITA kwa ajili ya kuhifadhiwa. Amefafanua kwamba japokuwa cheti kinachotolewa kinajazwa kwa mkono lakini ni nyaraka halali kabisa kwa matumizi yoyote na mtoto atakitumia miaka yote hata mpaka wakati wa uzee kutokana na jinsi Mungu atakavyomjalia kuishi hivyo amewasihi wananchi kuvitunza vyeti hivyo. Bw. Kanyusi amewashukuru wadau wa maendeleo wanaoshirikiana na Serikali katika utekelezaji wa Mpango wa Usajili wa Watoto. Wadau hao ni Serikali ya Canada, Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Kampuni ya simu za mkononi ya TIGO na kuwaomba kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuwasajili watoto na wananchi wote kwa ujumla.

**"Tunaamini kwamba kupitia Mpango huu Wakala utaweza kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, la kuhakikisha kila mtoto amesajiliwa kufikia mwisho wa mwaka 2025"**

*Frank Kanyusi - Kabidhi Wasihi Mkuu RITA*

# MASHAURI 705 YAOKOA TRILIONI 3.4



Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi akisoma hotuba wakati wa ufunguzi wa Baraza la pili la Wafanyakazi wa Ofisi yake. 2023/2024.

**Na Hyasinta Kissima**
**- WyKS Dodoma**

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kusimamia na kushinda Mashauri 705 yenye madai ya fedha na kuipelekea Serikali kuokoa zaidi ya Shilingi Trilioni 3.47 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024.

Mhe. Sagini ameyasema hayo Aprili 19, 2024 wakati akifungua kikao cha pili cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024 katika ukumbi wa mikutano wa NSSF, Mkoani Morogoro.

"Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeonesha uzalendo na weledi katika kuhahikisha Serikali inashinda katika Mashauri na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Fedha ambazo zimeokolewa ni mchango mkubwa katika kuisaidia Serikali kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Niwapongeze kwa hatua hii na niwasihi tuendelee kulipigania Taifa."Alisema Mhe. Sagini.

Aliendelea kusema "Tunaishukuru sana Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyoiwezesha Ofisi hii. Ongezeko la bajeti kutoka Shilingi Bilioni 17 zilizotengwa mwaka 2023/2024 hadi kufikia ukomo wa Shilingi Bilioni 20.7 kwa mwaka 2024/2025 ni ishara kubwa kwamba Mhe. Rais anatambua mchango mkubwa wa Ofisi hii katika kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri ya madai na usuluhishi"

Katika hatua nyingine Mhe Sagini amesema kupitia mikakati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya ardhi, Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi kwa kuishughulikia mapema kabla ya kuwasilishwa Mahakamani au katika mabaraza ya ardhi.

Kwa upande wake, Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende amesema kuwa Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo Watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ikiwemo mafunzo ya kiubobevu katika maeneo maalumu ambapo kwa kipindi cha Julai 2023, hadi Aprili 2024 jumla ya Watumishi 11 wamepatiwa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 56 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Aidha, Dkt. Luhende amesema upo uhitaji mkubwa wa Mawakili wenye ubobevu katika maeneo ya gesi,mafuta,uwekezaji,anga,-madini,uchumi wa bluu,TEHAMA ili kuiwezesha Ofisi hiyo kufanya vizuri zaidi katika maeneo hayo ya kimkakati.




Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa pili wa Baraza la Pili la Wafanyakazi kwa mwaka 2023/2024 wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo ameipongeza kwa hatua inayoendelea kuchukua katika kulitetea na kupigania maslahi ya Taifa.

# SERIKALI INAENDELEA KUIMARISHA **MISINGI YA HAKI NA UTAWALA BORA**




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akihutubia Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali, 21 Machi, 2024 Dodoma.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akifafanua jambo kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (hayupo pichani) alipotembelea banda la Wizara kabla ya kufungua Mkutano wa Mawakili wa Serikali, tarehe 21 Machi, 2024 Dodoma.*

**Na William Mabusi**
- WyKS Dodoma

”Serikali inaendelea kuchukua hatua za maksudi na madhubuti kuboresha mfumo wa haki jinai, kujenga mazingira wezeshi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria ya kutoa huduma za kisheria kwa wananchi kote nchini. Jukumu hilo la utoaji haki linafanyika pasipo kujali dini, rangi au itikadi ya siasa ya mtu kwani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu wote ni sawa mbele ya sheria na wote wanapashwa kulindwa na kupata haki sawa.”

Kauli ilitolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) alipokuwa anafungua Mkutano Mkuu wa siku tatu wa Mawakili wa Serikali tarehe 21 Machi, 2024 Jijini Dodoma.

Akiongelea uhitaji wa huduma ya sheria Mhe. Majaliwa amesema ”katika miaka ya hivi karibuni jamii imepitia mabadiliko na maendeleo mbalimbali katika maeneo ya kiuchumi, kiteknolojia, kiasiasa na kiutamaduni. Maendeleo hayo yameongeza uhitaji wa upatikanaji wa huduma za kisheria.”

Akihitimisha hotuba yake Mhe. Majaliwa aliwaagiza Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria kutekeleze majukumu yao ya kisheria kwa uadilifu, weledi, uwajibikaji, uaminifu, usiri, umakini na kwa kujituma huku akiwataka kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika kutekeleza kampeni ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia Lega Aid Campaign kwa kuipa uzito kama sehemu ya majukumu mengine ya kila siku.

Katika mkutano huo, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana aliyataja matunda ya kazi wanazofanya Mawakili wa Serikali. Katika miaka miwili ya kuwepo kwa Chama cha Mawakili wa serikali, Mhe.Balozi Dkt Pindi Chana alisema kuwa taifa limeshuhudia mchango mkubwa wa Mawakili wa Serikali ambao umewezesha ustawi wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, uwekezaji, utalii, uhusiano wa kimataifa, utoaji haki, utawala wa sheria, umoja wa kitaifa, na msaada wa kisheria,.

Akiongelea ushirikiano wa Serikali na Watetezi wa haki za Binadamu, Dkt. Chana amesema Serikali itaendelea kufanya kazi kwa pamoja na Mtandao wa Watetezi wa haki za binadamu kwa lengo moja la kuona Tanzania inaendelea kuwa na amani.




# USAJILI WA MASHIRIKA YANAYOTOA MSAADA WA KISHERIA

## Njia ya Usajili

- Usajili unafanyika kwa njia ya Mtandao
  Tembelea Tovuti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya *www.sheria.go.tz*, kisha bonyeza eneo la Huduma Mtandao, kisha chagua Usajili wa watoa huduma za Msaada wa Kisheria.

- Au ingia moja kwa moja kwenye anuani ya *https://legalaid.sheria.go.tz;* na Nenda sehemu iliyoandikwa **REGISTRATION** kisha tengeneza akaunti ya Shirika kisha fuata maelekezo kusajili Shirika.



# SERIKALI KUENDELEA KUIMARISHA MAJENGO NA HUDUMA ZA MAHAKAMA



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akijibu maswali Bungeni tarehe 02 Aprili, 2024 Jijini Dodoma.*

**Na William Mabusi**
- WyKS Dodoma

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amesema Serikali imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati majengo chakavu.

Dkt. Chana amesema hayo wakati akijibu maswali Bungeni tarehe 02 Aprili, 2024 Jijini Dodoma. "Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati majengo chakavu kwa awamu kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti."

Ameitaja Wilaya ya Mkalama kuwa moja ya Wilaya ambazo zimo kwenye mpango wa Mahakama zitakazojengwa katika Bajeti ya Mwaka 2023/24 ambapo maandalizi ya michoro ya Mahakama hiyo yamekamilika na zabuni imetangazwa ili kupata Mkandarasi wa ujenzi. Amezitaja Mahakama nyingine ambazo zimo kwenye mpango wa bajeti ya mwaka 2023/24 kuwa ni pamoja na Mahakama ya Wilaya ya Kishapu na Tarime.

Sambamba na ujenzi na ukarabati wa majengo, Mahakama imeanzisha kitengo maalum kushughulikia malalamiko ya Wananchi kufuatilia kesi zao kwa kupiga namba maalum 0752 500 400 ambapo watapata taarifa za kesi zao pamoja na kujibiwa malalamiko mengine.

Katika hatua nyingine Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana amesema nia ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuona Wananchi wanaendelea kupata haki kwa wakati. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeendelea kuboresha utoaji haki na kuimarisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Aidha, amesema Serikali itaendelea kutekeleza mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya haki za binadamu, kuendelea kutoa elimu ya haki za binadamu, wakati wote kuwa na sera za kutetea haki za binadamu na kuchukua hatua dhidi ya ukatili wa haki za binadamu.




*Jengo la Kituo Jumuishi cha utoaji Haki lililopo Dodoma ambaloni moja kati ya jitihada za Mahakama katikakuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali*

# Matumizi tekinolojia katika Mahakama



Mnamo Julai 11, 2024 Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini alikutana na kufanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kujifunza majukumu ya Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria.

**Na Hyasinta Kissima**
**- WyKS DSM**

Mnamo Julai 11, 2024 Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini alikutana na kufanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kuzitembelea na kujifunza majukumu ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Katika mazungumzo hayo yaliyotanguliwa na kulitembelea jengo la Makao Makuu ya Mahakama yaliyopo Tambukareli jijini Dodoma, Mhe. Jumanne Sagini alifurahishwa na maboresho makubwa yaliyofanywa na Mhimili wa Mahakama ikiwemo ujenzi wa jengo la Mahakama lenye Teknolojia na vifaa vya kisasa ambalo litakua miongoni mwa majengo makubwa sita bora Duniani lenye thamani ya Shilingi Bilioni 129.7.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel alisema kuwa, maboresho yanayofanywa katika Mhimili wa Mahakama kama vile upatikana wa vifaa vya kisasa, rasilimali watu, ujenzi wa miundombinu ya kisasa, matumizi ya TEHAMA, yameleta mchango mkubwa katika ubora wa utoaji haki Nchi na imani ya Wananchi kwa Mahakama imeongezeka maradufu.

“Nilipopewa jukumu la kumsaidia Mhe. Waziri Dkt. Balozi Pindi Chana katika Wizara ya Katiba na Sheria, nilisema lazima nijue hiki ninachoenda kukifanya. Tunapokea ripoti mbalimbali na tunazisoma. Lakini, ningeishia kwenye ripoti pekee bila kufika katika jengo hili na nimetembelea jengo hili sura ni tofauti kabisa. Alisema Sagini

Aliendelea kusema, “Nimeona makubwa kwenye TEHAMA. Jaji Mkuu aliniambia uje utembelee kwa kweli mna maajabu. Ninaweza kuona taarifa ya Mahakama ya Mkoa fulani, inafanya nini, shauri gani limepangwa kusikilizwa, mashahidi au hukumu inatolewa kwamba hiyo taarifa ninaweza kuipata hapa. Lakini malalamiko ya Wananchi kituo cha huduma kwa mteja kwamba kutakuwa na watu masaa 24 kusikiliza kero za Wananchi, na kuzitafutia masuluhisho, huu ni ubunifu mkubwa sana.”

Naibu Waziri Sagini amesema kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria inaimani na kazi kubwa inayofanywa na Mahakama na itaendelea kuisemea Mahakama katika majukwaa mbalimbali na pia kuitumia Mahakama kupitia maboresho yaliyofanyika kuwa sehemu ya eneo la kujifunza kwa Taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara na zinazohusika katika utoaji wa Haki kwa Wananchi.



Katika mazungumzo hayo yaliyotanguliwa na kulitembelea jengo la Makao Makuu ya Mahakama yaliyopo Tambukareli jijini Dodoma, Naibu alifurahishwa na maboresho makubwa yaliyofanywa na Mhimili wa Mahakama ikiwemo ujenzi wa jengo la Mahakama lenye Teknolojia na vifaa vya kisasa ambalo litakua miongoni mwa majengo makubwa sita bora Duniani lenye thamani ya Shilingi Bilioni 129.7




# Tanzania imeendelea kuvutia mikutano ya kimataifa

**Na William Mabusi**
- WyKS Dodoma

Mikakati mbalimbali inayofanywa na Serikali katika kusimamia haki za binadamu na watu imeifanya Tanzania kuendelea kuwavutia waandaaji wa mikutano ya kimataifa kufanya mikutano hiyo nchini. Katika kipindi cha miaka mitatu ya kuwa madarakani Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanyika mikutano mikubwa ya kimataifa Jijini Arusha na Zanzibar.

Oktoba 20, 2023 Jijini Arusha kilifanyika Kikao cha Kawaida cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambapo katika kikao hicho Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilimtunuku Tuzo ya Heshima Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wake katika kutetea, kulinda na kuimarisha haki za binadamu katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita ya Mhe. Dkt. Samia idadi ya wanawake katika vyombo vya utoaji maamuzi ikiwemo Mahakama, Bunge na Serikalini kwa ujumla imeongezeka.

Katika hatua nyingine kati ya Machi 04 hadi 08, 2024 kwa mara ya kwanza nchini ulifanyika Mkutano wa Mawaziri wa Sheria kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola, huko Zanzibar. Mkutano huo




Kikao cha 77 cha Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika AICC - Arusha

ulifunguliwa rasmi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali.

"Nashukuru Jumuiya ya Madola kwa kuchagua nchi yetu Tanzania na hasa hapa Zanzibar kufanyia mkutano huu mkubwa ambao unalenga kujadili pamoja na mambo mengine jinsi maendeleo ya kidijitali yanavyowezesha kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu." Alisema.

Akielezea mikakati mbalimbali inayofanywa na Serikali katika kusimamia utoaji haki alisema "Serikali ilizindua kampeni kubwa inayoitwa Mama Samia Legal Aid Campaign kushughulikia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria, upatikanaji wa haki kwa wananchi katika ngazi zote, kushughulikia masuala mtambuka yanayohusu haki za binadamu na watu, mapambano dhidi ya ukatili wa kinjinsia, ukatili dhidi ya wanawake na watoto, masuala ya usimamizi wa ardhi, mirathi na utatuzi wa migogoro."

Katika salaam zake kwenye Mkutano huo Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na aliyekuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alisema chini ya utawala wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa katika masuala ya uzingatiaji amani, demokrasia na maendeleo.



Wageni waliohudhuria kikao cha Jumuiya ya Madola wakifurahia vivutio Zanzibar

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola MH. Patricia Scotland KC akitoa salaam katika mkutano huo alitoa pole kwa Tanzania kwa kuondokewa na Rais wa Awamu ya Pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi akimtaja Mwinyi kama kiongozi aliyeleta mapinduzi katika teknolojia.

# Tanzania yasifiwa kwa kupokea na kuhifadhi wakimbizi



Kamishna Mkuu Msaidizi wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi UNHCR bwana Raouf Mazou, akimkabidhi zawadi Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana tarehe 04/07/2024 alipofika Ofisini kwake yalipo Makao Makuu ya Shirikika hilo Geneva, Switzerland.

**Na Lusajo Mwakabuku**
- WyKS Geneva

Tanzania imetajwa kuwa nchi ya mfano katika kuwapokea na kuwahifadhi wakimbizi toka enzi za Rais wa Awamu ya Kwanza Hayati Julius Kambarage Nyerere.

Hayo yameelezwa na Kamishna Mkuu Msaidizi wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi UNHCR bwana Raouf Mazou, alipofanya mazungumzo na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana leo tarehe 04/07/2024 Ofisini kwake yalipo Makao Makuu ya Shirikika hilo Geneva, Switzerland.

Kamishna Mazou aliongeza kuwa Tanzania ukilinganisha na nchi nyingine imekuwa ikipokea wakimbizi na kuwapatia mahitaji muhimu na pia akatumia nafasi hiyo kueleza umuhimu wa wanaoishi katika maeneo ya wakimbizi kupewa elimu bora ili wakirudi kwao waweze kujiendeleza pamoja na kuchangia katika maendeleo ya nchi zao.

Kwa upande wake Waziri Chana alisema serikali inaendelea na jitihada za kuongeza uhamasishaji katika maeneo ambayo wanaingilia wakimbizi kama ambavyo Mwalimu Nyerere alisema kuwa tofauti ni mipaka ila waafrika ni wamoja na pia akatoa mfano wa Rais Kabila ambaye naye alikuwa mkimbizi nchini Tanzania na akaweza kurudi nchini kwao na kuwa kiongozi.

Waziri Chana kwa upande wake alitumia nafasi hiyo Kumuomba Kamishna Mazou kuangalia nafasi zozote za ushirikiano katika masuala ya uwezeshaji kwa watu wanaowashughulikia wakimbizi nchini Tanzania.

**"Tanzania ukilinganisha na nchi nyingine kihistoria imekuwa ni nchi inayopokea wakimbizi na kuwapatia mahitaji muhimu kwa kipindi cha muda mrefu toka enzi za wapigania uhuru na kuifanya kuwa moja ya nchi zinazoheshimika katika kujali haki za binadamu"**

*Raouf Mazou - Kamishna Mkuu Msaidizi wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi (UNHCR)*




Kamishna Mkuu Msaidizi wa shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi UNHCR bwana Raouf Mazou, aakizungumza na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana na ujumbe wake Ofisini kwake Geneva Switzerland.

# Matukio katika Picha




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Mwinyi akizindua kikao cha 77 cha Tume ya Haki za Binadamu Ausha.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akipokea tuzo kutoka ACHPR kwa niaba ya Rais Samia.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akimnyanyua mtoto aliyeletwa na mzazi katika banda la RITA.*

*Vijana wakipiga "Makachu" ikiwa ni sehemu ya utalii kwa wageni wakati wa kikao cha Jumuiya ya Madola Zanzibar akiakikupokewa na viongozi wa Mkoa na Wizara*





*Naibu Katibu Mkuu wa MoCLA  Dkt. Khatib Kazungu akiongea na wakazi wa Makete katika utekelezaji wa MSLAC mkoani Njombe*



*Meza Kuu na Mawakili wa Serikali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya uzinduzi wa Kliniki ya sheria, Juni 26, 2024 Dodoma.*

